Tangazo La Serikali Na. 674 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA MAJALILA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Majalila ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

*Tangazo La Serikali Na. 674 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama P1 yenye majira - nukta 276360.20E, 9316861.77N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S28°00'17"E kwa umbali wa kilometa 1.99 hadi alama ya mpaka ya upimaji P2 yenye majira - nukta 277298.09E, 9315098.20N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini- Mashariki katika uelekeo wa N55°48'25"E kwa umbali wa kilomita 0.761 hadi alama ya mpaka ya upimaji P3 yenye majira - nukta 277927.72E, 9315525.98N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N29°40'43"W kwa umbali wa kilometa 2.02 hadi alama ya mpaka ya upimaji P2 yenye majira - nukta 276927.97E, 9317280.25N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Magharibi katika uelekeo wa S53°36'30"W kwa umbali wa kilomita 0.705 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*